


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

MSIMAMIZI WA UCHAGUZI

HALMASHAURI YA NACHINGWEA

JIMBO LA NACHINGWEA

Unapojuibu tafadhali taja:

Kumb. Na LG.E.50/1 VOL V/109

Tarehe 18 Sept, 2020

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA

Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la NACHINGWEA Kwa kuzingatia kanuni ya 14 ya kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 12 ya kanuni za Uchaguzi za Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020 anakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wenyе sifa na uwezo wa kujaza nafasi za Watendaji wa Uchaguzi Mkuu utakaofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020 kama ifuatavyo:-

1. **MSIMAMIZI WA KITUO CHA KUPIGA KURA (NAFASI 425)**
 2. **MSIMAMIZI MSAIDIZI WA KITUO CHA KUPIGA KURA (NAFASI 850)**
 3. **KARANI MWONGOZAJI WAPIGA KURA (NAFASI 425)**
- A. **SIFA ZA MWOMBAJI WA NAFASI YA MSIMAMIZI AU MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI**
- a. Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi,
 - b. Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa
 - c. Awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu
 - d. Awe amemaliza elimu ya kidato cha nne (4) au zaidi na anaweza kusoma na kuandika vizuri. Pia, anayeweza kuyaelewa maelekezo ya Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura na
 - e. Ikiwezekana awe mkazi wa kata ambayo anaomba
- B. **SIFA ZA WAOMBAJI WA NAFASI YA KARANI MWONGOZAJI WA WAPIGA KURA**
- (a) Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi.

- (b) Awe mkazi wa kata ambayo anafanyia kazi ya kuongoza wapiga kura
- (c) Awe wadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu.
- (d) Awe na elimu isiyopungua kidato cha nne na anayeweza kusoma na kuyaelewa maelekezo kwa Makarani Waongozaji Wapiga Kura; na
- (e) Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa.

C. MALIPO

Malipo yatakuwa kama ifuatavyo:-

- i. Msimamizi wa Kituo siku ya Uchaguzi atalipwa posho ya Tzs. 35,000 kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Tzs 15,000 kwa siku moja na nauli Tzs 20,000;
- ii. Msimamizi Msaidizi wa Kituo atalipwa posho ya Tzs. 30,000 kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Tzs 15,000 na nauli Tzs 20,000; na
- iii. Karani Mwongozaji Wapiga kura atalipwa posho ya Tzs. 30,000 kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Tzs 15,000.


D. MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE

- Waombaji waambatishe maelezo binafsi (Details C.V) yenyenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) wawili.
- Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kidato cha nne, kidato cha sita au kuhitimu mafunzo kwa kuzingatia sifa kwa mujibu wa Tangazo hili.
- Waombaji wambatanishe picha mbili za "Passort size" za hivi karibuni.
- Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wao.
- Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria.
- **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 27 Septemba, 2020.**

Anuani ya kutumia maombi ni:-

Msimamizi wa Uchaguzi,
 Jimbo la Uchaguzi Nachingwea,
 S.L.P 291,
NACHINGWEA.
TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA;

Hassan A Rugwa
Msimamizi wa Uchaguzi,
Jimbo la Uchaguzi
NACHINGWEA



NAKALA; 1. WATEMDAJI WA KATA WOTE,
NACHINGWEA - Bandikeni kwenye
MBAO za Matangazo.

2. MBAO ZA MATANGAZO HALMASHAURI YA
WILAYA YA NACHINGWEA.

